# USHIRIKA WA KIANGLIKANA

**Barua kwa Makanisa ya Ushirika wa Kianglikana toka kwa Maaskofu Wakuu wa Ushirika wa Kianglikana kufuatia Mkutano wao wa Dublin, Ireland, kati ya tarehe 24 na 30 Januari 2011**

Wakati wa mkutano wetu tulijadili hali na kuenea kwa ukatili wa kijinsia.[1] Tukijengea katika maazimio ya jambo hili wakati wa Halmashauri ya Majimbo ya Anglikana ya Africa (CAPA) [na] kongamano la maaskofu mwaka 2010, tulishirikishana masimulizi ya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana toka ukanda wa kusini na kaskazini mwa dunia, yakiwemo maelezo ya ngono za kikatili dhidi ya wanawake na wasichana katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ikiwa ni matokeo ya mgogoro, na maelezo ya unyanyasaji wa majumbani na aina nyingine nyingi za unyanyasaji katika nchi ya Uingereza na sehemu nyingine za dunia. Tunakiri kwa huzuni kuwa ukatili wa kijinsia ni tatizo la dunia nzima na ya kwamba asilimia yote ya ukatili japo ni kidogo inafanywa na wanaume dhidi ya wanawake, huku kukiwa na athari za kutisha kwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii.

Kwa kutafakari hali hii mbaya ya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, makanisa yetu lazima yakubali wajibu wake kwa sehemu yetu katika kuendeleza mitazamo ya ukandamizaji dhidi ya wanawake. Kwa majuto na imani lazima tusonge mbele katika namna ambayo makanisa yetu yatakuwa mashahidi wa kweli wa imani yetu, kwamba wote wanaume na wanawake wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Kuwaza na kuishi katika njia ambayo haionyeshi imani hii bali kuwaondolea uwezo na kuwatenga wengine, ni kuharibu mfano wa Mungu na kufanya uhalifu dhidi ya ubinadamu na Mungu.

Katika miaka ya hivi karibuni tumeona kukua kwa maafikiano katika Ushirika wa Kianglikana ili kujihusisha na utokomezaji wa ukatili wa kijinsia. Mnamo 2009 Halmashauri ya Ushauriano ya Anglikana (ACC) iliazimia kusaidia kuondoa ain azote za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana na kuhimiza Majimbo yote kushiriki katika mipango na matukio yanayokuza haki na ustawi wa mwanamke, kipekee kama inavyoelezwa katika mpango wa utekelezaji wa mkutano wa Beijing na Malengo ya Milenia. Pia ACC ilitoa mwito kwa makanisa kuchukua hatua za kufaa kusaidia uponyaji wa familia za wenyeji, ikiwemo kuwakinga wanawake na watoto dhidi ya ukatili na biashara ya kusafirisha binadamu.[2] Maaskofu walikutana katika Mkutano wa Lambeth wa 1998 and 2008 na kutafakari kuhusu ukatili ndani na nje ya Kanisa na kuomba makanisa kujihusisha na kukuza uwelewa wa umma kuhusu unyanyasaji na dhuluma kwa wanawake na watoto. Tuligundua kwamba mitandao kadhaa ilyo rasmi ya Kianglikana imeweka unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto kuwa jambo la kipaumbele kwa washariki wao na kwa wengine katika Ushirika mpana zaidi wa Kianglikana.

---

[1] Imeelezwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1993 kama '…ukatili usababishao, au unaoweza kusababisha madhara au mateso katika mwili, kijinsi au kisaikolojia kwa mwanamke, ikiwa ni pamoja na vitisho vinavyofanana na matendo haya ya kulazimisha au kumnyima uhuru hadharani au katika maisha ya faradha.'

[2] Maazimio ya ACC la 14.33: Mtandao wa Kimataifa wa Wanawake Waanglikana, na la 14.19: Mtandao wa Wanglikana Wenyeji

Tulitiwa moyo kufahamu kwamba kuna kiwango kikubwa cha kazi inayofanyika katika Ushirika wa Kianglikana kwa kadri makanisa yanavyojishughulisha na kukuza uelewa, utetezi, kubadili mtazamo na tabia zinazopelekea ukatili, kuwatunza na kuwarejesha katika jamii wahanga na waliookolewa katika ukatili, na kuwashughulikia watekelezaji wa ukatili. Tunamshukuru Mungu kwa jitihada hizi na tunazifurahia, na tunajitoa kwa moyo kuimarisha utume na huduma yetu katika maeneo haya.

Kwa kusudi hili tumemuomba Katibu Mkuu wa Ushirika wa Kanisa Anglikana Ulimwenguni, kwa kushirikiana na Mitandao hiyo na Shirikisho la Kianglikana, kuendelea kufuatia shughulia ambazo tayari zinajibu suala la ukatili wa kijinsia, na kutambua raslimali za kitheologia na kiutendaji na kutafakari jinsi raslimali hizi zinavyoweza kutumiwa na wengi kwa marejeo na kwa matumizi yanayoendana na mazingira mengine ya mahali husika.

Kila mmoja wetu tukiwa Maaskofu Wakuu tunajitoa kwa moyo, katika kila Jimbo letu, kukuza uelewa wa Lengo la 3 la Milenia ('Kukuza usawa wa kijinsia na kuwajengea uwezo wanawake'); kuamini na kuomba baraka za Mungu kwa shughuli ambazo tayari zinaendelea katika madayosisi na maparishi ili kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana; kuwakusanya pamoja viongozi wa makanisa na imani nyingine ili kutafakari nini tunachoweza kusema na kufanya pamoja; na kuhudhuria mafunzo ya wachungaji ili wawe na uelewa kuhusu hali na nguvu ya ukatili wa kijinsia na jinsi tunavyoweza kuukabili na kubadili mitazamo na tabia kadha wa kadhaa. Pia tunajitoa kwa moyo kuhakikisha uandaaji na upatikanaji wa vifaa, ikiwemo liturgia, kwa mfano, kwa ajili ya tarehe 25 Novemba ambayo kwa kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake, kadhalika ni Siku ya Utepe Mweupe,[3] na ni siku ya kwanza kwa ulimwengu ya ' Siku 16 ya Harakati ya Utokomezaji wa Ukatili dhidi ya Wanawake'. Zaidi ya hayo, kwa mafundisho na kielelezo, tutafanya kazi na vijana wetu ili kuona wavulana na wasichana wetu, vijana wa kiume na wakike, wamewezeshwa kujiheshimu wenyewe na wengine kama binadamu wanaothaminiwa katika hali ya usawa na Mungu, na wemejengewa uwezo kuwa vyanzo vya mabadiliko miongoni mwa marika wao.

[3] Utepe Mweupe ni kikundi cha wanaume na vijana kinachopambana na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.